APPEL DE GENÈVE
GENEVA CALL

info@genevacall.org
www.genevacall.org



© *Design: Kathleen Morf*

APPEL DE GENÈVE
GENEVA CALL

# Kanuni kuu kuhusu tabia ya wapiganaji wakati wa mapigano ya ndani



Swahili




1 Usishambulie raia, mali za raia au majengo ya umma ya kiraia



2

Usifaye mashambulio yoyote ikiwa hasara kwa raia itakuwa kubwa kuliko mafanikio ya kijeshi



3

Chukua tahadhari zinazotakiwa kuwalinda raia kabla, na wakati wa kufanya mashambulio





4 Usitumie silaha zilizokatazwa na usitumie mbinu za kivita zilizopigwa marufuku



5

Wakusanye na kuwatunza majeruhi na maiti, wawe ni wa upande wako au adui





6

Heshimu haki za wafungwa na watu wengine wote walio chini ya himaya yako na uwatunze kama binadamu

Usiue mtu kwa tuhuma tu, bila kutenda haki



7 Usiwashike watu mateka au kutumia binadamu kama ngao





8

Usiwahamishe raia kwa lazima, ikiwa sio kwa ajili ya usalama wao au kwa sababu kubwa za kijeshi



9

Heshimu mali ya raia

Usipore au kuiba



10

Waheshimu wanawake. Usibake au kuruhusu ubakaji, au unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya mtu yeyote





11

Walinde watoto

Usiwaandikishe katika majeshi yako
na usiwatumie kwenye hali ya vita







Waheshimu wahudumu wa kimatibabu, hospitali na magari ya wagonjwa

Usitumie vibaya nembo za kujilinda kama zile za shirika la Msalaba Mwekundu au Red Crescent



13

**Ruhusu ugavi wa misaada kwa raia wenye mahitaji pasipo upendeleo**




14

Zingatia kanuni hizi. Ziheshimu kanuni hizi hata kama adui anazikiuka

Jiepushe na kulipiza kwa sababu ni kinyume na sheria katika vita




15

Zuia ukiukwaji wa kanuni hiziw
Ikiwa ukiukwaji unatokea,
mfahamishe kamanda wako

Ukiukwaji wa kanuni lazima uchunguzwe
na kuadhibiwa kwa mujibu
wa viwango vya kimataifa

APPEL DE GENÈVE
GENEVA CALL

## Geneva Call

Geneva Call ni shirika lisilo la kiserikali, lisiloegemea upande wowote, na ambalo hujihusisha katika kufanya mashauriano na makundi yenye silaha yasiyotoka serikalini, katika kuhimiza kuzingatiwa na kuheshimiwa kwa kanuni za kimataifa kuhusu utoaji wa misaada ya kibinadamu.

Shirika la Geneva Call linaelekeza utendaji wake kwenye ulinzi wa raia walio kwenye mazingira ya vita, na hususan:

- Usalama wa watoto
- Kuzuia unyanyasaji wa kimapenzi na kuondoa ubaguzi wa kijinsia
- Kupigwa marufuku mabomu ya kutegwa ardhini kwa nia ya kujeruhi

## *Hati ya Ahadi*

*Hati za Ahadi* ni nyaraka rasmi zinazotiwa sahihihi na wadau katika mizozo, ambao hawatoki serikalini, wakiahidi kuheshimu kanuni za kimataifa za utoaji msaada wa kibinadamu.

Hadi kufikia sasa, shirika la Geneva Call limeandaa aina tatu za nyaraka hizo:

- *Hati ya kuahidi* kuzingatia kupigwa marufuku mabomu ya kutegwa ardhini kwa nia ya kujeruhi, na kutoa ushirikiano katika juhudi za kutegua mabomu kama hayo
- *Hati ya kuahidi* Kuwalinda Watoto kutokana na athari za mapigano
- *Hati ya kuahidi* kuzingatia kupigwa marufuku unyanyasaji wa kimapenzi kwenye mazingira ya vita na kuondolea mbali ubaguzi wa kijinsia

Shirika la Geneva Call huunga mkono na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa hizo Hati za Ahadi na makundi yenye silaha, yasiyo ya serikali, yaliyotia sahihi.